HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA
SHULE YA SEKONDARI KARIAKOO
S.L.P 275,
TABORA
January, 2019.

Simu Na. 0753671896 / 0786611665 / Mkuu wa shule
0762892122/ 0656207960 M/Mkuu wa shule
E.MAIL. kariakoosekondari@gmail.com

Kumb .Na.S.3113/J/F.I/2021/15

Kwa Mr./Mis ……
S.L.P ……

YAH: KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA 2021

1.0 UTANGULIZI

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya Sekondari kidato cha kwanza 2021, katika shule ya Sekondari Kariakoo, **KARIBU SANA**.
Shule hii ipo umbali wa km 03 ukitokea mjini katikati, ukiwa upande wa kusini fuata barabara ya Shule ya Sekondari Tabora wavulana na kufuata barabara iendayo Seminari kuu ya Kipalapala. Shule iko upande wa kushoto mara tu ukipita machinjioni.

Ukitumia usafiri wa pikipiki nauli ni shilingi elfu moja hadi elfu mbili. Shule itafunguliwa tarehe **11/1/2021,** na unatakiwa kuripoti shuleni siku hiyo na mwisho wa kuripoti ni tarehe **21 Januari, 2021**. Ni lazima ufike siku husika kabla ya saa 9:00 mchana na kupokelewa.
Utapokelewa shuleni utakapokuwa umetimiza mambo yaliyo kwenye viambatanisho **A – E.**

A: Maelezo Maalum ya Kuzingatia
B: Sheria za Shule
C: Fomu ya Kujiandikisha
D: Fomu ya kuripoti ya kupimwa Hospitali
E: kivuli cha cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate)

Ni matumaini yangu kuwa utasoma na kuzingatia maelezo yaliyotolewa. Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga katika Shule hii .

……
NYASEBWA LEONARD
MKUU WA SHULE

Enc:

KIAMBATANISHO A: MAELEZO MAALUM YA KUZINGATIA

2.0 SARE NA MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI

Shule hii ni shule ya Kutwa , hivyo kila mwanafunzi anapaswa kuwa na mahitaji yafuatayo:
Sare ya shule hii ni rangi ya ugoro kwa wavulana na wasichana

Maelezo ya Sare kwa wavulana :
Unapaswa kuwa na suruali mbili (2), Mashono , ziwe na malinda mawili na ziwe ndefu mpaka kugusa kisigino na kuvaliwa na mkanda mweusi .

NB: Mkanda usiwe na nembo yeyote au chuma kikubwa. Mikanda ya mabegi hairuhusiwi.

a) Aina ya kitambaa cha suruali na sketi: **YA RANGI YA UGORO**
b) Jozi mbili au zaidi za soksi nyeusi .

ONYO: Suruali za kubana mwili, modo, mtepesho na mdomo wa chupa kwa wavulana haziruhusiwi na hii ni **AMRI** .
Ukionekana umevaa suruali kinyume na makatazo hayo hapo juu itachanwa hapo hapo kwa **mkasi** .
Mzazi zingatia hili ndiyo maadili ya Taifa letu .
. **c)** Mashati mawili (2) meupe tetroni ya mikono mifupi na yavaliwe na Tai ya Tai ya rangi ya ugoro .

Maelezo ya Sare kwa wasichana :
a) Sketi mbili (2) , Mishono ya sketi ni linda boksi yenye malinda manne mbele mawili, nyuma mawili na pembeni mawili, Mshono kama wanavyoshona masista, ziwe ndefu kuvuka magoti nchi saba , Sketi fupi haziruhusiwi na hii ni **AMRI** .

b) Mashati mawili (2) meupe tetroni , ya mikono mifupi yavaliwe na Tai ya rangi ya Ugoro .

c) Kwa wasichana wanaotumia **Hijabu,** rangi ya Hijabu iwe nyeupe. Shona Juba

Maelekezo ya sare kwa wanafunzi wote wavulana na wasichana
Kila mwanafunzi anapaswa kuwa na

- Viatu vyeusi jozi moja au zaidi vya ngozi vyenye kutumia rangi (kiwi) nyeusi
- Sweta mbili au moja yenye rangi ya ugoro,lisiwe na mistari yoyote, masweta yanafanana kwa wanafunzi wote (makoti hayaruhusiwi)
- Sare ya michezo kwa shule hii ni T.shrt za rangi ya **Zambarau** kwa wavulana na wasichana **,** zinapatikana shuleni zikiwa tayari na Nembo ya shule mbele na nyuma

- Jozi mbili au zaidi za soksi nyeupe.
- Aje na daftari kumi (10) , kubwa Quire 3 au 4 , Mkebe wa hesabu (Mathematical set) , rula pia anatakiwa kuwa na begi la kubebea madaftari
- Aje na picha tatu (3) passport size apige akiwa amevaa shati jeupe la shule
- Aje namba ya simu ya mzazi /Mlezi halisi na afahamu mtaa/kitongoji anapoishi na wazazi / walezi wake

CHAKULA CHA MCHANA :
Wazazi wote wa kidato cha kwanza hadi cha nne watafanya kikao chao cha kwanza tarehe **28/1/2021** saa 3:00 asubuhi na kupitia kikao hiki wazazi watapanga mikakati ya chakula kwa mwaka 2021

KIAMBATANISHO B: SHERIA / TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE

2:1 Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978.
Pamoja na marekebisho yake kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995.
Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini, Wizara ya Elimu,Sayansi , Teknolojia na Mafunzo ya ufundi ,yenye dhamana na Elimu nchini na Ofisi ya Rais yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu hapa nchini .

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni.

HESHIMA:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mwanafunzi anatakiwa kuiheshimu bendera ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Nembo ya Taifa na Wimbo wa Taifa.

ONYO NA MARUFUKU: Mwanafunzi haruhusiwi kwa mazingira yeyote yale kuwa na makundi ya watu wa mtaani (magenge ya watu wa mtaani wenye tabia mbaya) , ikidhibitika na ukabainika kuwa una makundi ya vijana wa mtaani utasimamishwa masomo mara moja

MAHUDHURIO:

(a) Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria shule kila siku ya masomo na anawajibika kuhudhuria vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa ni **LAZIMA** , mwanafunzi atakayebainika kutoroka vipindi na kuwa na utoro wa rejareja hatua kali

zitachukuliwa ikiwemo mwanafunzi na wazazi / walezi wake kushitakiwa katani .

(b) Ni marufuku kupiga kelele au kusumbua darasani na kutoka nje ya darasa bila ruhusa ya mwalimu.

(c) Mwanafunzi unapaswa kuwahi shuleni na kuhudhuria paredi ya shule saa **1.00** kamili asubuhi , kwa siku zote za masomo, na kuwahi katika shughuli za shule na nyingine zote utakazopangiwa .

(d) Mwanafunzi anapaswa kutii kengele ya shule kulingana na utaratibu au ratiba ya shule na dharura zinazojitokeza.

(e) Mwanafunzi anapaswa kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za shule.

(f) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu ,maelekezo ya walimu .

Ni **MARUFUKU** mwanafunzi kuondoka shuleni muda wa masomo kabla hujaruhusiwa au bila ya kibali cha maandishi kutoka kwa mwalimu wa zamu au mlezi wa darasa kabla ya **8:30** mchana.

(g) Kutunza usafi wa mwili , mavazi , eneo maalumu alilopangiwa kufanya usafi (**special area**)

(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

(i) kutunza mali ya shule nay a wanafunzi wenzake

SARE:

(a) Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare ya shule ya Kariakoo sekondari ,wakati wote akiwa shuleni. Wanafunzi wavulana wanapaswa **kuchomekea** shati muda wote awapo shuleni.

(b) Nguo za michezo, ni T.shrt za **zambarau** ambazo zinapatikana shuleni zikiwa na Nembo ya shule

UNADHIFU:

(a) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na ndevu

(b) Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa chochote masikioni, shingoni wala mkononi isipokuwa saa.

(c) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na nywele ndefu au kunyoa mitindo au kuweka dawa nywele. Nywele ziwe na urefu wa kitana kidogo.

(d) Mwanafunzi anatakiwa kuwa safi wakati wote awapo shule au awapo nje ya shule

MAZINGIRA:

(a) Kila mwanafunzi katika miaka yote hapa shuleni atatakiwa kupanda na kukuza mti mmoja wa kudumu

(b) Kila mwanafunzi atagawiwa eneo lake **maalum** (Special Area) ambalo atalitunza kwa usafi mpaka atakapomaliza shule

(c) Kila mwanafunzi atakuwa na zamu ya usafi katika D darasa na , Vyoo vya shule .

MAENEO YASIYORUHUSIWA KUFIKA MWANAFUNZI:

(a) Mwanafunzi haruhusiwi kufika/kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu.
   i) Ofisi za Shule
   ii) Stoo za Shule
   iii) Maabara
   iv) Jikoni
   v) Baa, Kilabu au sehemu yoyote panapouzwa vileo **(MARUFUKU)** hata kama ni nje ya shule
   vi) Nyumba za wageni **(MARUFUKU)**
   vii) Nyumba za walezi bila sababu maalumu
   viii) Kutoka nje ya eneo la shule kabla ya saa 2.30 mchana /Alasiri bila ruhusa maalum.

2:2 MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA.

i) Wizi wa mali / vitu vya wanafunzi wenzake na umma
ii) Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule
iii) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma
iv) Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
v) Uasherati na ushoga
vi) Ubakaji
vii) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
viii) Kupigana au kupiga shuleni au nje ya shule
ix) Kuoa au kuolewa
x) Kukataa adhabu kwa makusudi
xi) Kutoa lugha chafu/matusi kwa walezi na wanafunzi wenzake
xii) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na **SIMU YA MKONONI au** vifaa vyovyote vinavyohusiana**.** (Kama sim card na charger, (**NI AMRI & MARUFUKU**)

Mzazi unatakiwa kutoa ushirikiano kwa hili, mshauri mtoto wako vizuri kuzingatia agizo hili bila kuleta sababu zozote.

MAMBO MENGINE MUHIMU ANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI ANAPORIPOTI

1. Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali au Kituo cha Afya cha Serikali . Fomu hii itakabidhiwa kwa M/Shule mara anaporipoti shuleni

2. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na Mkataba wa mwanafunzi na mzazi / mlezi kukubaliana na sheria , kanuni na maelekezo ya shule .

Taadhali soma kwa makini maelezo / maagizo hayo na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII

KIAMBATANISHO C:

1.Jina la Mwanafunza ……
2.Tarehe ya Kuzaliwa ……Mwezi:……Mwaka……
3.Amezaliwa katika
Wilaya……Mkoa……
4.Uraia ……
5.Shule ya msingi alikosoma ……
6.Mahali anapoishi kwa sasa……
i) Wilaya……
ii) Tarafa……
iii) Kata……
iv) Mtaa/Kitongoji/Kijiji……
7. Dini na Dhehebu ……
8. Jina la Mzazi/Mlezi……
a) Kazi ya mzazi / mlezi ……
b) Anwani ya Mzazi/Mlezi……
Mabadiliko yawasilishwe ofisini mara moja
c) Simu ya (Nyumbani/Mkononi) ya mzazi / mlezi tu

……
d) (Ni muhimu kwa mawasiliano ya dharura kati ya mzazi na walimu)

9. Unataarifiwa kuwa shule hii ni shule ya Serikali wala **siyo** ya **DINI** Fulani. Aidha inazingatia katiba ya nchi kuhusu uhuru wa kuabudu.
Hivyo, katika ratiba ya shule kuna vipindi maalumu vya dini, pia kila siku ya Ijumaa, wanafunzi huruhusiwa kwenda sehemu za ibada kulingana na imani zao.
Hivyo, Wanafunzi hawaruhusiwi kuanzisha ratiba yao ya kuabudu katikati ya vipindi na ratiba zingine za shule.

10. AHADI YA MWANAFUNZI
Mimi……
Ninakubali/Sikubali nafasi niliyopewa Naahidi/Siahidi kutii kikamilifu kanuni, Sheria na maagizo ya shule na ndiyo mwongozo wangu mpaka kumaliza Shule.

Sahihi ya Mwanafunzi: ……

11. AHADI YA MZAZI
Mimi Mzazi/Mlezi……Nakubaliana/Sikubaliani na maagizo yaliyotolewa hapo juu.
Jina la
Mzazi/Mlezi:……Tarehe:……

NB: Mwanafunzi anaporipoti shuleni ni **LAZIMA** aje na fomu hii ikiwa imejazwa kikamilifu.

KIAMBATANISHO D:
KARIAKOO SECONDARY SCHOOL

STUDENT'S MEDICAL CERTIFICATE "E"

(To be completed by the Government Medical Officer and return to the Headmaster, Kariakoo Secondary School)

Name**:** ……

Please exam the student named above and comment in his health by responding to the following items. Kindly put a tick (√) in front of either **YES** or **NO** whichever is applicable.

A: **Sight?** If YES State	**1** NO	**2** YES
B**: Hearing:** If YES State	**1** NO	**2** YES
C**: T.B.** If YES State	**1** NO	**2** YES
D: **Blood Pressure** If YES State	**1** NO	**2** YES
E: **ASTHMA**	**1** NO	**2** YES
F: An other health problems	**1** NO	**2** YES
G: Any physical Disability? If YES State	**1** NO	**2** YES

Do you therefore recommend the said student medically fit for student Ship at this school?

1. NO
2. YES

If No please state:……

Name and signature:……Designation:……

Date……
Official Stamp……

KIAMBATANISHO E:
beMwanafunzi aje na nakala ya Cheti cha kuzaliwa iliyothibitishwa.